

**MAJIBU YENYE FAIDA**

**NO. 11**

**KUHUSU**

**MASWALI YA MIFUMO MIPYA**

**MTUNZI: SHEIKH SWALEH BIN FAZAN AL FAWZAN**

**MFASIRI: UMAR BIN MUHAMMAD BIN KONDO**

**PONGWE – TANGA- TANZANIA**

## **Swali la kumi na nne.**

Miongoni mwa yanayojulikana ni kwamba, kulingania kwenye dini ya Allah kunahitaji Elimu ya kisheria,je..! basi (makusudio ya Elimu kwa hapa ) ni hii Elimu ya kuhifadhi kitabu cha Allah(Qur'an) na sunna (Hadithi sahihi)?

Na je..! itatosha Elimu ambayo inasomwa katika madrasa na vuyo vikuu kwa ajili ya kulingania kwenye Dini ya Allah?

**Jawabu:** Elimu (inayokusudiwa) ni kuhifadhi Nusuusi (maandiko ya wazi) na kufahamu maana zake, na haitatosha kuhifadhi maandiko tu, haitoshi kuwa mtu anahifadhi maandiko ya Qur'an na Hadithi tu, hapana budi kujua maana zake sahihi, ama kuhifadhi maandiko tu bila ya

kufahamu maana zake,hili hailimuwezshi mtu kustahiki kulingania kwenye Dini ya Allah .

Ama yale yanayosomeshwa shulen (madrasa) ikiwa katika madrasa hizo kuna kuhifadhi nusuus (maandiko ya wazi) na kufahamu maana zake, basi hili linatosha (kulingania).

Ama ikiwa ni kuhifadhi maandiko bila ya kufahamu maana,basi hili halitamuwezesha mtu kulingania,lakini (pamwe na hayo) linalowezekana kwenye hili awahifadhishe watu maandiko ambayo ameyahifadhi na awakaririshe maandiko hayo bila ya kufafanua maana zake au awasomee na awasikilizishe maandiko hayo.

